

Jinsi ya kupika Eggchop

By SW - Melkisedeck Shine · December 2, 2022

Dondoo za Mapishi na Lishe · Upishi na Maandalizi ya Milo yenye Afya · #Karibu AckySHINE

Mahitaji

Mayai yaliochemshwa 4 Nyama ya kusaga robo kilo Kitunguu swaum Tangawizi Limao Chumvi
Pilipili Breadcrumbs Carry powder Binzari nyembamba ya unga Yai moja bichi Mafuta

Matayarisho

Marinate nyama na pilipili, kitunguu swaum, tangawizi, limao, chumvi, carry powder, binzari nyembamba na breadcrumbs pamoja. Kisha vunja yai moja bichi kwenye kibakuli na ulikoroge kisha tia kwenye mchanganyiko wa nyama. Gawanisha matonge manne kwa ajili ya kuzungushia kwenye mayai. Chemsha mayai kwa muda wa dakika 20. Yakisha iva acha yapoe na kisha yamenye maganda na uyaweke pembeni. Baada ya hapo chukua yai moja lililochemshwa na ulizungushie donge moja la mchanganyiko wa nyama. fanya hivyo kwa mayai yote yaliobakia. Baada ya hapo paka mafuta kwa nje ya hizo eggchop na kisha paka mafuta kwenye sinia la kuokea na uziokoe kwenye oven kwa moto wa kawaida, kwa muda wa dakika 20. Na eggchop zako zitakuwa tayari kwa kuliwa

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=24750>